TOLEO NA. 08

# TOLEO LATAKWIMU ZA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII - ZANZIBAR KWA MWEZI WA APRILI - JUNI, 2026


IMETAYARISHWA NA

KITENGO CHA TAKWIMU ZA MATUKIO YA KIJAMII

JULAI 2026

## 1.0 Utangulizi

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa utaratibu wa utekelezaji wa majukumu yake iliyojipangia katika kuimarisha takwimu za Matukio ya Kijamii. Miongoni mwa takwimu hizo ni takwimu za Usajili wa Vizazi, Vifo, Ndoa na Talaka.

Toleo la robo ya pili ya mwaka 2026 (April-Juni), linatoa muhtasari wa takwimu za Matukio ya kijamii. Takwimu hizi zinatolewa kwa mlinganisho wa kijiografia (Wilaya) na kijinsia. Takwimu za Matukio ya Kijamii hutoa taarifa za idadi ya matukio ya kijamii yaliyosajiliwa na Wakala wa Usajili na Matukio ya Kijamii Zanzibar.

## 2.0 Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za Usajili wa Matukio ya Kijamii za ndani ya Zanzibar. Upatatikaji wa taarifa hizi ni muhimu katika kupanga maendeleo ya kijamii, kupima mafanikio ya Sera za Afya na kutambua changamoto za kijamii. Aidha, takwimu za matukio ya Kijamii husaidia katika kutathimini maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi, pia hutoa mwongozo muhimu kwa watafiti, serikali, na mashirika ya maendeleo katika kufanya tathimini na maamuzi sahihi kwa jamii. Toleo hili linawasilisha takwimu zifuatazo.

### 2.1 Vizazi Vilivyosajiliwa Aprili-Juni, 2026.

Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa jumla ya vizazi hai 7,936 vilisajiliwa katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026, ambapo wanaume walikuwa 4,162 (52.4%) na wanawake 3,774 (47.6%). Kwa mujibu wa miezi, mwezi wa Aprili vilisajiliwa vizazi 2,367 (29.8%), vikijumuisha wanaume 1,242 (52.5%) na wanawake 1,125 (47.5%); mwezi wa Mei vilisajiliwa vizazi 3,090 (38.9%), vikijumuisha wanaume 1,669 (54.0%) na wanawake 1,421 (46.0%); huku mwezi wa Juni vilisajiliwa vizazi 2,479 (31.2%), vikijumuisha wanaume 1,251 (50.5%) na wanawake 1,228 (49.5%). Hali hii inaonesha kuwa usajili wa vizazi hai uliongezeka kutoka Aprili hadi Mei, kisha ukapungua mwezi Juni, huku wanaume wakisajiliwa kwa idadi kubwa kuliko wanawake katika miezi yote ya kipindi husika.

Kwa ngazi ya wilaya, Jedwali Na. 1 linaonesha kuwa Wilaya ya Wete iliongoza kwa

kusajili vizazi hai 1,303 (16.4%), ikifuatiwa na Mjini vizazi 1,171 (14.8%), Magharibi B vizazi 929 (11.7%) na Micheweni vizazi 890 (11.2%), huku Wilaya ya Kaskazini B ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vizazi 135 (1.7%). Kwa ujumla, wilaya nyingi zilionesha idadi kubwa ya wanaume kuliko wanawake, ingawa baadhi ya wilaya kama Kaskazini A, Kati na Magharibi A zilikuwa na wanawake wengi zaidi kuliko wanaume katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026.

**Jadweli Na. 1: Usajili wa Vizazi Hai kwa Jinsi na Wilaya, Aprili-Juni, 2026**

| Wilaya | Aprili-2026 | | | Mei-2026 | | | Juni-2026 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 120 | 127 | **247** | 151 | 145 | **296** | 119 | 154 | **273** | 390 | 426 | **816** |
| Kaskazini B | 19 | 21 | **40** | 21 | 21 | **42** | 21 | 32 | **53** | 61 | 74 | **135** |
| Kati | 85 | 87 | **172** | 82 | 80 | **162** | 76 | 77 | **153** | 243 | 244 | **487** |
| Kusini | 74 | 69 | **143** | 51 | 39 | **90** | 76 | 72 | **148** | 201 | 180 | **381** |
| Mjini | 155 | 139 | **294** | 269 | 224 | **493** | 223 | 161 | **384** | 647 | 524 | **1,171** |
| Magharibi A | 66 | 61 | **127** | 95 | 107 | **202** | 96 | 91 | **187** | 257 | 259 | **516** |
| Magharibi B | 203 | 133 | **336** | 307 | 179 | **486** | 47 | 60 | **107** | 557 | 372 | **929** |
| Micheweni | 114 | 95 | **209** | 188 | 182 | **370** | 168 | 143 | **311** | 470 | 420 | **890** |
| Wete | 184 | 170 | **354** | 280 | 246 | **526** | 195 | 228 | **423** | 659 | 644 | **1,303** |
| Chakechake | 146 | 152 | **298** | 159 | 130 | **289** | 131 | 138 | **269** | 436 | 420 | **856** |
| Mkoan | 76 | 71 | **147** | 66 | 68 | **134** | 99 | 72 | **171** | 241 | 211 | **452** |
| **Jumla** | **1,242** | **1,125** | **2,367** | **1,669** | **1,421** | **3,090** | **1,251** | **1,228** | **2,479** | **4,162** | **3,774** | **7,936** |

## 2.1 Uwiano wa Kijinsia kwa Usajili wa Vizazi Hai

Jadweli Na. 2 linaonesha kuwa katika kipindi cha Aprili–Juni 2026, jumla ya vizazi hai 7,936 vilisajiliwa, ambapo wanaume walikuwa 4,162 (52.4%) na wanawake 3,774 (47.6%). Hivyo, uwiano wa kijinsia ulikuwa 110.3, ikimaanisha kuwa kulikuwa na takribani watoto wa kiume 110 kwa kila watoto wa kike 100 waliosajiliwa.

Kwa ngazi ya wilaya, Magharibi B ilikuwa na uwiano wa kijinsia mkubwa zaidi wa 149.7, ikifuatiwa na Mjini (123.5), Mkoani (114.2), Micheweni (111.9) na Kusini (111.7), hali inayoonesha kuwa watoto wa kiume walikuwa wengi kuliko wa kike katika wilaya hizo. Kwa upande mwingine, Kaskazini B ilikuwa na uwiano wa kijinsia mdogo zaidi wa 82.4, ikifuatiwa na Kaskazini A (91.5), jambo linaloonesha kuwa watoto wa kike walikuwa wengi kuliko wa kiume katika wilaya hizo.

Aidha, Kati (99.6) na Magharibi A (99.2) zilikuwa karibu na uwiano wa 100, zikionesha uwiano wa karibu sawa kati ya watoto wa kiume na wa kike waliosajiliwa. Kwa ujumla, wilaya nyingi zilikuwa na uwiano wa kijinsia unaozidi 100, ikimaanisha kuwa vizazi vya watoto wa kiume vilikuwa vingi kuliko vya watoto wa kike katika kipindi cha Aprili–Juni 2026.

**Jadweli Na. 2: Uwiano wa Kijinsia wa Usajili wa Vizazi Hai kwa Wilaya, Aprili–Juni 2026.**

| Wilaya | Apr-26 | Mei-2026 | Juni-2026 | April-Juni, 2026 Uwianao wa Kijinsia |
|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 390 | 426 | 816 | 91.5 |
| Kaskazini B | 61 | 74 | 135 | 82.4 |
| Kati | 243 | 244 | 487 | 99.6 |
| Kusini | 201 | 180 | 381 | 111.7 |
| Mjini | 647 | 524 | 1,171 | 123.5 |
| Magharibi A | 257 | 259 | 516 | 99.2 |
| Magharibi B | 557 | 372 | 929 | 149.7 |
| Micheweni | 470 | 420 | 890 | 111.9 |
| Wete | 659 | 644 | 1,303 | 102.3 |
| Chakechake | 436 | 420 | 856 | 103.8 |
| Mkoani | 241 | 211 | 452 | 114.2 |
| Jumla | **4,162** | **3,774** | **7,936** | **110.3** |

### 2.1.2 Mlinganisho wa Vizazi Hai vilivyosajiliwa Januari–Machi, 2026 na Aprili-Juni, 2026

Jedwali Na. 3 linaonesha kuwa jumla ya vizazi hai 7,936 vilisajiliwa katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026, ikilinganishwa na vizazi 12,758 vilivyosajiliwa katika kipindi cha Januari hadi Machi 2026. Hii ni sawa na upungufu wa vizazi 4,822 (37.8%). Katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026, wanaume walikuwa 4,162 (52.4%) na wanawake 3,774 (47.6%), wakati Januari hadi Machi 2026 wanaume walikuwa 6,137 (48.1%) na wanawake 6,621 (51.9%). Hii inaonesha kuwa usajili wa vizazi hai ulipungua kwa kiasi kikubwa katika robo ya pili ya mwaka, huku uwiano wa jinsia ukibadilika kutoka wanawake kuwa wengi zaidi katika robo ya kwanza hadi wanaume kuwa wengi zaidi katika robo ya pili.

Kwa ngazi ya wilaya, katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026, Wilaya ya Wete ilisajili idadi kubwa zaidi ya vizazi hai 1,303 (16.4%), ikifuatiwa na Mjini vizazi 1,171 (14.8%),

Magharibi B vizazi 929 (11.7%) na Micheweni vizazi 890 (11.2%), huku Kaskazini B ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vizazi 135 (1.7%).

Ikilinganishwa na kipindi cha Januari hadi Machi 2026, karibu wilaya zote zilionesha kupungua kwa usajili wa vizazi hai katika Aprili hadi Juni 2026. Upungufu mkubwa zaidi ulirekodiwa Wilaya ya Magharibi A, ambapo usajili ulipungua kutoka vizazi 1,259 hadi 516 (upungufu wa 59.0%), ukifuatiwa na Mkoani kutoka 1,134 hadi 452 (upungufu wa 60.1%), Kaskazini B kutoka 353 hadi 135 (upungufu wa 61.8%) na Chakechake kutoka 1,367 hadi 856 (upungufu wa 37.4%). Hata hivyo, Wilaya ya Wete ndiyo pekee iliyoonesha ongezeko la usajili wa vizazi hai, kutoka vizazi 1,222 hadi 1,303, sawa na ongezeko la asilimia 6.6.

Kwa upande wa jinsia, kipindi cha Januari hadi Machi 2026 kilikuwa na wanawake wengi zaidi kuliko wanaume katika wilaya nyingi. Hata hivyo, katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026 hali ilibadilika, ambapo wanaume walikuwa wengi zaidi katika wilaya nyingi isipokuwa Kaskazini A, Kaskazini B, Kati na Magharibi A, ambazo zilisajili wanawake wengi zaidi kuliko wanaume. Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kupungua kwa kiwango cha usajili wa vizazi hai katika robo ya pili ya mwaka 2026 ikilinganishwa na robo ya kwanza, huku Wilaya ya Wete ikiwa pekee iliyofanikiwa kuongeza idadi ya usajili wa vizazi hai.

**Jadweli Na. 3: Mlinganisho wa Vizazi Hai vilivyosajiliwa Januari–Machi, 2026 na Aprili-Juni, 2026**

| Wilaya | Januari-Machi, 2026 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 644 | 668 | **1,312** | 390 | 426 | **816** |
| Kaskazini B | 168 | 185 | **353** | 61 | 74 | **135** |
| Kati | 282 | 271 | **553** | 243 | 244 | **487** |
| Kusini | 284 | 284 | **568** | 201 | 180 | **381** |
| Mjini | 1052 | 1188 | **2,240** | 647 | 524 | **1,171** |
| Magharibi A | 612 | 647 | **1,259** | 257 | 259 | **516** |
| Magharibi B | 668 | 787 | **1,455** | 557 | 372 | **929** |
| Micheweni | 619 | 676 | **1295** | 470 | 420 | **890** |
| Wete | 592 | 630 | **1,222** | 659 | 644 | **1,303** |
| Chakechake | 638 | 729 | **1367** | 436 | 420 | **856** |
| Mkoani | 578 | 556 | **1,134** | 241 | 211 | **452** |
| **Jumla** | **6,137** | **6,621** | **12,758** | **4,162** | **3,774** | **7,936** |

### 2.1.1 Mlinganisho wa Vizazi Hai vilivyosajiliwa Aprili–June, 2025 na Aprili-Juni, 2026

Jumla ya vizazi hai 7,936 vilisajiliwa katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026 ikilinganishwa na vizazi 10,062 vilivyosajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Hii ni sawa na upungufu wa vizazi 2,126 (21.1%). Kati ya vizazi vilivyosajiliwa mwaka 2026, wanaume walikuwa 4,162 (52.4%) na wanawake 3,774 (47.6%), wakati mwaka 2025 wanaume walikuwa 5,183 (51.5%) na wanawake 4,879 (48.5%). Hali hii inaonesha kuwa wanaume walisajiliwa kwa idadi kubwa kuliko wanawake katika vipindi vyote viwili.

Kwa ngazi ya wilaya, mwaka 2026 Wilaya ya Wete ilisajili idadi kubwa zaidi ya vizazi hai 1,303 (16.4%), ikifuatiwa na Mjini vizazi 1,171 (14.8%), Magharibi B vizazi 929 (11.7%), na Micheweni vizazi 890 (11.2%) huku Kaskazini B ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vizazi 135 (1.7%).

Ikilinganishwa na kipindi cha Aprili hadi Juni 2025, wilaya nyingi zilipungua katika idadi ya vizazi vilivyosajiliwa mwaka 2026. Upungufu mkubwa ulijitokeza Wilaya ya Mjini, ambapo usajili ulipungua kutoka vizazi 2,557 hadi 1,171 (upungufu wa 54.2%), ukifuatiwa na Magharibi A kutoka 1,058 hadi 516 (upungufu wa 51.2%), Magharibi B kutoka 1,242 hadi 929 (upungufu wa 25.2%) na Micheweni kutoka 1,008 hadi 890 (upungufu wa 11.7%). Hata hivyo, baadhi ya wilaya zilionesha ongezeko la usajili wa vizazi hai, hususan Wilaya ya Kati kutoka vizazi 353 hadi 487 (ongezeko la 38.0%), Kaskazini B kutoka vizazi 96 hadi 135 (ongezeko la 40.6%), Chakechake kutoka 784 hadi 856 (ongezeko la 9.2%), Kaskazini A kutoka 778 hadi 816 (ongezeko la 4.9%) na Kusini kutoka 378 hadi 381 (ongezeko dogo la 0.8%).

Kwa upande wa jinsi, mwaka 2026 wilaya nyingi zilisajili wanaume wengi kuliko wanawake. Hata hivyo, Kaskazini A, Kaskazini B, Kati na Magharibi A zilikuwa na wanawake wengi zaidi kuliko wanaume, wakati wilaya nyingine zilikuwa na wanaume wengi kuliko wanawake. Hali hii inaonesha kuwa pamoja na kupungua kwa jumla ya usajili wa vizazi hai mwaka 2026, tofauti za usajili kati ya wilaya ziliendelea kuwepo, huku baadhi ya wilaya zikionesha mwenendo wa ongezeko na nyingine zikipata upungufu mkubwa wa usajili, Jedwali Na. 4.

**Jadweli Na. 4: Mlinganisho wa Vizazi Hai vilivyosajiliwa Aprili–June, 2025 na Aprili-Juni, 2026**

| Wilaya | Aprili-Juni, 2025 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 377 | 401 | 778 | 390 | 426 | **816** |
| Kaskazini B | 46 | 50 | 96 | 61 | 74 | **135** |
| Kati | 180 | 173 | 353 | 243 | 244 | **487** |
| Kusini | 187 | 191 | 378 | 201 | 180 | **381** |
| Mjini | 1,341 | 1,216 | 2,557 | 647 | 524 | **1,171** |
| Magharibi A | 552 | 506 | 1,058 | 257 | 259 | **516** |
| Magharibi B | 647 | 595 | 1,242 | 557 | 372 | **929** |
| Micheweni | 515 | 493 | 1,008 | 470 | 420 | **890** |
| Wete | 693 | 626 | 1,319 | 659 | 644 | **1,303** |
| Chakechake | 415 | 369 | 784 | 436 | 420 | **856** |
| Mkoani | 230 | 259 | 489 | 241 | 211 | **452** |
| **Jumla** | **5,183** | **4,879** | **10,062** | **4,162** | **3,774** | **7,936** |

### 2.1.2 Usajili wa Vizazi Hai Ndani ya Wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari – Machi, 2026

Jadweli Na. 5 linaonesha kuwa jumla ya vizazi hai 6,207 vilisajiliwa ndani ya wakati katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026, ambapo wanaume walikuwa 3,382 (54.5%) na wanawake 2,856 (46.0%). Kwa mujibu wa miezi, mwezi Aprili vizazi 1,924 (31.0%) vilisajiliwa, vikijumuisha wanaume 1,042 (54.2%) na wanawake 882 (45.8%); mwezi Mei vizazi 2,498 (40.2%) vilisajiliwa, vikijumuisha wanaume 1,395 (55.8%) na wanawake 1,103 (44.2%); huku mwezi Juni vizazi 1,785 (28.8%) vilisajiliwa, vikijumuisha wanaume 945 (52.9%) na wanawake 871 (48.8%). Hali hii inaonesha kuwa usajili wa vizazi hai uliongezeka kutoka mwezi Aprili hadi Mei, kisha ukapungua mwezi Juni, huku wanaume wakisajiliwa kwa idadi kubwa kuliko wanawake katika miezi yote ya kipindi husika.

Kwa ngazi ya wilaya, Jadweli Na. 5 linaonesha kuwa Wilaya ya Mjini iliongoza kwa kusajili vizazi hai 1,085 (17.5%), ikifuatiwa na Wete vizazi 1,077 (17.4%), Magharibi B vizazi 848 (13.7%) na Chakechake vizazi 692 (11.1%), huku Wilaya ya Kaskazini B ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vizazi 60 (1.0%). Kwa ujumla, wilaya nyingi zilionesha idadi kubwa ya

wanaume kuliko wanawake katika usajili wa vizazi ndani ya wakati katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026.

**Jadweli Na. 5: Usajili wa Vizazi Hai Ndani ya Wakati kwa Jinsi na Wilaya, Aprili – Juni, 2026**

| Wilaya | Aprili-2026 | | | Mei-2026 | | | Juni-2026 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 102 | 86 | **188** | 116 | 113 | **229** | 119 | 113 | **201** | 337 | 312 | **618** |
| Kaskazini B | 6 | 2 | **8** | 14 | 12 | **26** | 8 | 18 | **26** | 28 | 32 | **60** |
| Kati | 68 | 73 | **141** | 70 | 62 | **132** | 58 | 64 | **122** | 196 | 199 | **395** |
| Kusini | 67 | 66 | **133** | 44 | 30 | **74** | 72 | 68 | **140** | 183 | 164 | **347** |
| Mjini | 147 | 127 | **274** | 254 | 206 | **460** | 206 | 145 | **351** | 607 | 478 | **1,085** |
| Magharibi A | 46 | 45 | **91** | 76 | 80 | **156** | 80 | 70 | **150** | 202 | 195 | **397** |
| Magharibi B | 187 | 112 | **299** | 296 | 167 | **463** | 43 | 43 | **86** | 526 | 322 | **848** |
| Micheweni | 82 | 74 | **156** | 113 | 104 | **217** | 72 | 60 | **132** | 267 | 238 | **505** |
| Wete | 168 | 144 | **312** | 238 | 194 | **432** | 162 | 171 | **333** | 568 | 509 | **1,077** |
| Chakechake | 120 | 114 | **234** | 137 | 111 | **248** | 105 | 105 | **210** | 362 | 330 | **692** |
| Mkoan | 49 | 39 | **88** | 37 | 24 | **61** | 20 | 14 | **34** | 106 | 77 | **183** |
| **Jumla** | **1042** | **882** | **1,924** | **1395** | **1103** | **2498** | **945** | **871** | **1785** | **3,382** | **2,856** | **6,207** |

### 2.1.3 Mlinganisho wa Vizazi Hai vilivyosajiliwa ndani ya wakati, Januari–Machi, 2026 na Aprili-Juni, 2026

Jadweli Na. 6 linaonesha kuwa jumla ya vizazi hai 10,751 vilisajiliwa ndani ya wakati katika kipindi cha Januari–Machi 2026, ikilinganishwa na vizazi 6,207 vilivyosajiliwa katika kipindi cha Aprili–Juni 2026. Hii ni upungufu wa vizazi 4,544, sawa na asilimia 42.3. Katika kipindi cha Januari–Machi, 2026 wanawake walikuwa 5,685 (52.9%) na wanaume 5,066 (47.1%), wakati katika kipindi cha Aprili–Juni, 2026 wanaume walikuwa 3,382 (54.5%) na wanawake 2,856 (46.0%). Hali hii inaonesha kuwa usajili wa vizazi hai ndani ya wakati ulipungua kwa kiasi kikubwa katika robo ya pili ya mwaka, huku uwiano wa jinsia ukibadilika kutoka wanawake kuwa wengi katika robo ya kwanza hadi wanaume kuwa wengi katika robo ya pili.

Kwa ngazi ya wilaya, Wilaya ya Wete ndiyo pekee iliyoonesha ongezeko la usajili, kutoka vizazi 1,058 katika Januari–Machi, 2026 hadi 1,077 katika Aprili–Juni, 2026 ikiwa ni ongezeko la vizazi 19 (1.8%). Wilaya ya Kati pia ilibaki karibu na kiwango kilekile,

ikiongezeka kidogo kutoka 386 hadi 395 (asilimia 2.3). Wilaya zote zilizobaki zilionesha upungufu wa usajili. Upungufu mkubwa zaidi ulirekodiwa Mkoani, ambapo usajili ulishuka kutoka 820 hadi 183 (asilimia 77.7), ikifuatiwa na Kaskazini B kutoka 174 hadi 60 (asilimia 65.5), Magharibi A kutoka 1,119 hadi 397 (asilimia 64.5) na Mjini kutoka 2,154 hadi 1,085 (asilimia 49.6). Wilaya nyingine zilipungua kwa viwango tofauti, zikiwemo Chakechake (37.6%), Kusini (36.8%), Micheweni (41.6%) na Magharibi B (38.8%). Mwenendo huu unaashiria kupungua kwa usajili wa vizazi hai ndani ya wakati katika robo ya pili ya mwaka 2026 katika karibu wilaya zote za Zanzibar.

**Jadweli Na. 6: Mlinganisho wa Vizazi Hai vilivyosajiliwa ndani ya wakati, Januari–Machi, 2026 na Aprili-Juni, 2026**

| Wilaya | Januari-Machi, 2026 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 541 | 591 | **1,132** | 337 | 312 | **618** |
| Kaskazini B | 90 | 84 | **174** | 28 | 32 | **60** |
| Kati | 191 | 195 | **386** | 196 | 199 | **395** |
| Kusini | 270 | 279 | **549** | 183 | 164 | **347** |
| Mjini | 1,005 | 1,149 | **2,154** | 607 | 478 | **1,085** |
| Magharibi A | 538 | 581 | **1,119** | 202 | 195 | **397** |
| Magharibi B | 637 | 748 | **1,385** | 526 | 322 | **848** |
| Micheweni | 405 | 460 | **865** | 267 | 238 | **505** |
| Wete | 498 | 560 | **1,058** | 568 | 509 | **1,077** |
| Chakechake | 500 | 609 | **1,109** | 362 | 330 | **692** |
| Mkoani | 391 | 429 | **820** | 106 | 77 | **183** |
| **Jumla** | **5,066** | **5,685** | **10,751** | **3,382** | **2,856** | **6,207** |

### 2.1.4 Usajili wa Vizazi Hai Nje ya Wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari – Machi, 2026

Jadweli Na. 7 linaonesha kuwa jumla ya vizazi hai 1,729 vilisajiliwa nje ya wakati katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2026, ambapo wanaume walikuwa 811 (46.9%) na wanawake 918 (53.1%). Kwa mujibu wa miezi, mwezi Aprili vilisajiliwa vizazi 443 (25.6%), vikijumuisha wanaume 200 (45.1%) na wanawake 243 (54.9%); mwezi Mei vilisajiliwa vizazi 592 (34.2%), vikijumuisha wanaume 274 (46.3%) na wanawake 318 (53.7%); huku mwezi Juni vikisajiliwa vizazi 694 (40.1%), vikijumuisha wanaume 337 (48.6%) na wanawake 357 (51.4%). Hali hii inaonesha kuwa usajili wa vizazi hai nje ya wakati uliongezeka mfululizo kutoka mwezi Aprili hadi Juni, huku wanawake wakisajiliwa

kwa idadi kubwa kuliko wanaume katika miezi yote ya kipindi husika.

Kwa ngazi ya wilaya, Jadweli Na. 7 linaonesha kuwa Wilaya ya Micheweni iliongoza kwa kusajili vizazi hai 385 (22.3%) nje ya wakati, ikifuatiwa na Mkoani vizazi 269 (15.6%), Wete vizazi 226 (13.1%), Kaskazini A vizazi 198 (11.5%) na Chakechake vizazi 164 (9.5%), huku Wilaya ya Kusini ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vizazi 34 (2.0%) vilivyosajiliwa nje ya wakati. Kwa ujumla, wilaya nyingi zilionesha idadi kubwa ya wanawake kuliko wanaume katika usajili wa vizazi nje ya wakati katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2026.

**Jadweli Na. 7: Usajili wa Vizazi Hai Nje ya Wakati kwa Jinsi na Wilaya, Aprili – Juni, 2026**

| Wilaya | Aprili-2026 | | | Mei-2026 | | | Juni-2026 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 18 | 41 | **59** | 35 | 32 | **67** | 119 | 41 | **72** | 172 | 114 | **198** |
| Kaskazini B | 13 | 19 | **32** | 7 | 9 | **16** | 13 | 14 | **27** | 33 | 42 | **75** |
| Kati | 17 | 14 | **31** | 12 | 18 | **30** | 18 | 13 | **31** | 47 | 45 | **92** |
| Kusini | 7 | 3 | **10** | 7 | 9 | **16** | 4 | 4 | **8** | 18 | 16 | **34** |
| Mjini | 8 | 12 | **20** | 15 | 18 | **33** | 17 | 16 | **33** | 40 | 46 | **86** |
| Magharibi A | 20 | 16 | **36** | 19 | 27 | **46** | 16 | 21 | **37** | 55 | 64 | **119** |
| Magharibi B | 16 | 21 | **37** | 11 | 12 | **23** | 4 | 17 | **21** | 31 | 50 | **81** |
| Micheweni | 32 | 21 | **53** | 75 | 78 | **153** | 96 | 83 | **179** | 203 | 182 | **385** |
| Wete | 16 | 26 | **42** | 42 | 52 | **94** | 33 | 57 | **90** | 91 | 135 | **226** |
| Chakechake | 26 | 38 | **64** | 22 | 19 | **41** | 26 | 33 | **59** | 74 | 90 | **164** |
| Mkoan | 27 | 32 | **59** | 29 | 44 | **73** | 79 | 58 | **137** | 135 | 134 | **269** |
| **Jumla** | **200** | **243** | **443** | **274** | **318** | **592** | **337** | **357** | **694** | **811** | **918** | **1,729** |

### 2.1.3 Mlinganisho wa Vizazi Hai vilivyosajiliwa nje ya wakati, Januari–Machi, 2026 na Aprili-Juni, 2026

Jadweli Na. 8 linaonesha kuwa jumla ya vizazi hai 2,007 vilisajiliwa nje ya wakati katika kipindi cha Januari–Machi 2026, ikilinganishwa na vizazi 1,729 vilivyosajiliwa katika kipindi cha Aprili–Juni 2026. Hii ni upungufu wa vizazi 278, sawa na asilimia 13.9. Katika kipindi cha Januari–Machi, wanaume walikuwa 1,071 (53.4%) na wanawake 936 (46.6%), wakati katika kipindi cha Aprili–Juni wanaume walikuwa 811 (46.9%) na wanawake 918 (53.1%). Hali hii inaonesha kuwa usajili wa vizazi hai nje ya wakati ulipungua katika robo

ya pili ya mwaka 2026, huku uwiano wa jinsia ukibadilika kutoka wanaume kuwa wengi katika robo ya kwanza hadi wanawake kuwa wengi katika robo ya pili.

Kwa ngazi ya wilaya, Wilaya ya Wete ilionesha ongezeko kubwa zaidi la usajili wa vizazi nje ya wakati, kutoka vizazi 164 katika kipindi cha Januari–Machi hadi 226 katika Aprili–Juni, ikiwa ni ongezeko la vizazi 62 (37.8%). Wilaya nyingine zilizoonesha ongezeko ni Kaskazini A, kutoka 180 hadi 198 (asilimia 10.0), Kusini, kutoka 19 hadi 34 (asilimia 78.9), na Magharibi B, kutoka 70 hadi 81 (asilimia 15.7), huku Mjini ikibaki katika kiwango kilekile cha vizazi 86 katika vipindi vyote viwili.

Wilaya zilizobaki zilionesha upungufu wa usajili wa vizazi nje ya wakati. Upungufu mkubwa zaidi ulirekodiwa Wilaya ya Kaskazini B, ambapo usajili ulishuka kutoka 179 hadi 75 (asilimia 58.1), ikifuatiwa na Wilaya ya Kati, kutoka 167 hadi 92 (asilimia 44.9), Chakechake, kutoka 258 hadi 164 (asilimia 36.4) na Mkoani, kutoka 314 hadi 269 (asilimia 14.3). Mwenendo huu unaashiria kuwa, licha ya baadhi ya wilaya kuonesha ongezeko la usajili wa vizazi nje ya wakati, kwa ujumla usajili huo ulipungua katika robo ya pili ya mwaka 2026 ikilinganishwa na robo ya kwanza.

**Jadweli Na. 8: Mlinganisho wa Vizazi Hai vilivyosajiliwa nje ya wakati, Januari–Machi, 2026 na Aprili-Juni, 2026**

| Wilaya | Januari-Machi, 2026 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 103 | 77 | **180** | 172 | 114 | **198** |
| Kaskazini B | 78 | 101 | **179** | 33 | 42 | **75** |
| Kati | 91 | 76 | **167** | 47 | 45 | **92** |
| Kusini | 14 | 5 | **19** | 18 | 16 | **34** |
| Mjini | 47 | 39 | **86** | 40 | 46 | **86** |
| Magharibi A | 74 | 66 | **140** | 55 | 64 | **119** |
| Magharibi B | 31 | 39 | **70** | 31 | 50 | **81** |
| Micheweni | 214 | 216 | **430** | 203 | 182 | **385** |
| Wete | 94 | 70 | **164** | 91 | 135 | **226** |
| Chakechake | 138 | 120 | **258** | 74 | 90 | **164** |
| Mkoani | 187 | 127 | **314** | 135 | 134 | **269** |
| **Jumla** | **1,071** | **936** | **2,007** | **811** | **918** | **1,729** |

### 3.1 Vifo Vilivyosajiliwa Aprili-Juni, 2026.

Jedwali Na. 9 linaonesha kuwa jumla ya vifo 547 vilisajiliwa katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026, ambapo wanaume walikuwa 346 (63.3%) na wanawake 201 (36.7%). Kwa mujibu wa miezi, mwezi wa Aprili vilisajiliwa vifo 197 (36.0%), vikijumuisha wanaume 127 (64.5%) na wanawake 70 (35.5%); mwezi wa Mei vilisajiliwa vifo 192 (35.1%), vikijumuisha wanaume 123 (64.1%) na wanawake 69 (35.9%); huku mwezi wa Juni vilisajiliwa vifo 158 (28.9%), vikijumuisha wanaume 96 (60.8%) na wanawake 62 (39.2%). Hali hii inaonesha kuwa usajili wa vifo ulipungua kwa mfululizo kutoka mwezi Aprili hadi Juni, huku wanaume wakisajiliwa kwa idadi kubwa kuliko wanawake katika miezi yote ya kipindi husika.

Kwa ngazi ya wilaya, Jedwali Na. 9 linaonesha kuwa Wilaya ya Mjini iliongoza kwa kusajili vifo 129 (23.6%), ikifuatiwa na Chakechake vifo 69 (12.6%), Magharibi B vifo 68 (12.4%) na Magharibi A na Mkoani vifo 51 kila moja (9.3%), huku Wilaya ya Kusini ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vifo 17 (3.1%). Kwa ujumla, wilaya zote zilionesha idadi kubwa ya vifo vya wanaume kuliko wanawake isipokuwa Wilaya ya Wete, ambapo wanawake 15 walikuwa wengi kuliko wanaume 13 katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026.

**Jadweli Na. 9: Usajili wa Vifo kwa Jinsi na Wilaya, Aprili-Juni, 2026**

| Wilaya | Aprili-2026 | | | Mei-2026 | | | Juni-2026 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 10 | 8 | **18** | 12 | 3 | **15** | 119 | 5 | **15** | 32 | 16 | **48** |
| Kaskazini B | 6 | 6 | **12** | 8 | 2 | **10** | 2 | 1 | **3** | 16 | 9 | **25** |
| Kati | 4 | 3 | **7** | 7 | 4 | **11** | 7 | 4 | **11** | 18 | 11 | **29** |
| Kusini | 4 | 3 | **7** | 2 | 2 | **4** | 3 | 3 | **6** | 9 | 8 | **17** |
| Mjini | 27 | 14 | **41** | 34 | 19 | **53** | 23 | 12 | **35** | 84 | 45 | **129** |
| Magharibi A | 13 | 8 | **21** | 9 | 8 | **17** | 5 | 8 | **13** | 27 | 24 | **51** |
| Magharibi B | 22 | 13 | **35** | 15 | 7 | **22** | 8 | 3 | **11** | 45 | 23 | **68** |
| Micheweni | 4 | 2 | **6** | 9 | 5 | **14** | 9 | 3 | **12** | 22 | 10 | **32** |
| Wete | 4 | 1 | **5** | 3 | 6 | **9** | 6 | 8 | **14** | 13 | 15 | **28** |
| Chakechake | 21 | 9 | **30** | 10 | 9 | **19** | 13 | 7 | **20** | 44 | 25 | **69** |
| Mkoan | 12 | 3 | **15** | 14 | 4 | **18** | 10 | 8 | **18** | 36 | 15 | **51** |
| **Jumla** | **127** | **70** | **197** | **123** | **69** | **192** | **96** | **62** | **158** | **346** | **201** | **547** |

## 2.1 Uwiano wa Kijinsia kwa Usajili wa Vifo

Jadweli Na. 10 linaonesha kuwa kwa kipindi cha Aprili–Juni 2026, jumla ya vifo 547 vilisajiliwa, ambapo wanaume walikuwa 346 (63.3%) na wanawake 201 (36.7%). Hivyo, uwiano wa kijinsia ulikuwa 172.1, ikimaanisha kuwa kulikuwa na takribani vifo vya wanaume 172 kwa kila vifo 100 vya wanawake vilivyosajiliwa katika kipindi hicho.

Kwa ngazi ya wilaya, Mkoani ilikuwa na uwiano wa kijinsia mkubwa zaidi wa 240, ikifuatiwa na Micheweni (220), Kaskazini A (200), Magharibi B (195.7) na Mjini (186.7). Hali hii inaonesha kuwa vifo vya wanaume vilikuwa vingi zaidi kuliko vya wanawake katika wilaya hizo. Aidha, Wete ilikuwa wilaya pekee iliyokuwa na uwiano wa kijinsia chini ya 100 (86.7), jambo linaloonesha kuwa vifo vya wanawake vilikuwa vingi kuliko vya wanaume katika wilaya hiyo. Aidha, Kusini na Magharibi A zilikuwa na uwiano wa kijinsia wa 112.5, ukionesha tofauti ndogo kati ya vifo vya wanaume na wanawake.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa katika wilaya nyingi za Zanzibar kulikuwa na uwiano wa kijinsia unaozidi 100, jambo linaloashiria kuwa vifo vya wanaume vilikuwa vingi kuliko vya wanawake katika kipindi cha Aprili–Juni 2026. Hali hii pia imejidhihirisha katika kiwango cha Zanzibar kwa ujumla, ambapo uwiano wa kijinsia ulifikia 172.1.

**Jadweli Na. 10: Uwiano wa Kijinsia wa Usajili wa Vifo kwa Wilaya, Aprili–Juni 2026.**

| Wilaya | Apr-26 | Mei-2026 | Juni-2026 | April-Juni, 2026 Uwianao wa Kijinsia |
|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 32 | 16 | 48 | 200.0 |
| Kaskazini B | 16 | 9 | 25 | 177.8 |
| Kati | 18 | 11 | 29 | 163.6 |
| Kusini | 9 | 8 | 17 | 112.5 |
| Mjini | 84 | 45 | 129 | 186.7 |
| Magharibi A | 27 | 24 | 51 | 112.5 |
| Magharibi B | 45 | 23 | 68 | 195.7 |
| Micheweni | 22 | 10 | 32 | 220.0 |
| Wete | 13 | 15 | 28 | 86.7 |
| Chakechake | 44 | 25 | 69 | 176.0 |
| Mkoani | 36 | 15 | 51 | 240.0 |
| Jumla | **346** | **201** | **547** | **172.1** |

### 2.1.2 Mlinganisho wa Vifo vilivyosajiliwa Januari–Machi, 2026 na Aprili-Juni, 2026

Jedwali Na. 11 linaonesha kuwa jumla ya vifo vilivyosajiliwa vilipungua kutoka 655 katika kipindi cha Januari–Machi 2026 hadi 547 katika kipindi cha Aprili–Juni 2026, sawa na upungufu wa vifo 108 (16.5%). Katika kipindi cha Januari–Machi 2026, wanaume walikuwa 417 (63.7%) na wanawake 238 (36.3%), wakati katika kipindi cha Aprili–Juni 2026 wanaume walikuwa 346 (63.3%) na wanawake 201 (36.7%). Hali hii inaonesha kuwa idadi ya vifo ilipungua katika kipindi cha Aprili–Juni 2026, huku wanaume wakiendelea kuwa na idadi kubwa ya vifo kuliko wanawake katika vipindi vyote viwili.

Kwa ngazi ya wilaya, Wilaya ya Mjini ilisajili idadi kubwa zaidi ya vifo katika vipindi vyote viwili, ikipungua kutoka vifo 142 katika Januari–Machi hadi vifo 129 katika Aprili–Juni. Wilaya nyingi zilionesha kupungua kwa idadi ya vifo, zikiwemo Kaskazini A (67 hadi 48), Kusini (47 hadi 17), Magharibi A (66 hadi 51), Micheweni (34 hadi 32) na Wete (62 hadi 28), ambapo Wete ilionesha upungufu mkubwa zaidi wa vifo 34. Hata hivyo, baadhi ya wilaya zilionesha ongezeko dogo la vifo, zikiwemo Kaskazini B (16 hadi 25), Chakechake (61 hadi 69), na Mkoani (50 hadi 51), wakati Magharibi B ilishuhudia upungufu mdogo kutoka 72 hadi 68. Kwa ujumla, mabadiliko haya yanaonesha kupungua kwa usajili wa vifo katika wilaya nyingi kati ya vipindi hivi viwili, ingawa baadhi ya wilaya ziliendelea kurekodi ongezeko la vifo.

**Jadweli Na. 11: Mlinganisho wa Vifo vilivyosajiliwa Januari–Machi, 2026 na Aprili-Juni, 2026**

| Wilaya | Januari-Machi, 2026 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 47 | 20 | **67** | 32 | 16 | **48** |
| Kaskazini B | 10 | 6 | **16** | 16 | 9 | **25** |
| Kati | 25 | 13 | **38** | 18 | 11 | **29** |
| Kusini | 22 | 25 | **47** | 9 | 8 | **17** |
| Mjini | 91 | 51 | **142** | 84 | 45 | **129** |
| Magharibi A | 46 | 20 | **66** | 27 | 24 | **51** |
| Magharibi B | 38 | 34 | **72** | 45 | 23 | **68** |
| Micheweni | 25 | 9 | **34** | 22 | 10 | **32** |
| Wete | 44 | 18 | **62** | 13 | 15 | **28** |
| Chakechake | 34 | 27 | **61** | 44 | 25 | **69** |
| Mkoani | 35 | 15 | **50** | 36 | 15 | **51** |
| **Jumla** | **417** | **238** | **655** | **346** | **201** | **547** |

### 2.1.4 Mlinganisho wa Vifo vilivyosajiliwa Aprili – Juni, 2025 na Aprili – Juni, 2026

Jadweli Na. 12 linaonesha kuwa katika kipindi cha Aprili–Juni 2025, jumla ya vifo 467 vilisajiliwa, ambapo wanaume walikuwa 285 (61.0%) na wanawake 182 (39.0%), hali inayoonesha kuwa vifo vya wanaume vilikuwa vingi zaidi kuliko vya wanawake. Wilaya ya Mjini iliongoza kwa kusajili vifo 126 (27.0%), ikifuatiwa na Mkoani 51 (10.9%), Chakechake 46 (9.9%), Magharibi A 45 (9.6%), na Kati 41 (8.8%), huku Wilaya ya Kaskazini B ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vifo 12 (2.6%). Takwimu hizi zinaonesha kuwa zaidi ya robo ya vifo vyote vilivyosajiliwa katika kipindi hicho vilitokea Wilaya ya Mjini.

Katika kipindi cha Aprili–Juni 2026, jumla ya vifo 547 vilisajiliwa, ikiwa ni ongezeko la vifo 80 (17.1%) ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2025. Katika kipindi hicho, wanaume walikuwa 346 (63.3%) na wanawake 201 (36.7%), hali inayoonesha kuwa wanaume waliendelea kuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika usajili wa vifo. Wilaya ya Mjini iliendelea kuongoza kwa kusajili vifo 129 (23.6%), ikifuatiwa na Chakechake 69 (12.6%), Magharibi B 68 (12.4%), Magharibi A 51 (9.3%), na Mkoani 51 (9.3%), huku Wilaya ya Kusini ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vifo 17 (3.1%).

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa usajili wa vifo uliongezeka kwa asilimia 17.1 katika kipindi cha Aprili–Juni 2026 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2025. Aidha, wanaume waliendelea kuwa na idadi kubwa zaidi ya vifo vilivyosajiliwa katika vipindi vyote viwili. Wilaya ya Mjini iliendelea kuwa na mchango mkubwa zaidi wa vifo katika miaka yote miwili, ingawa mchango wake kwa jumla ya vifo ulipungua kutoka asilimia 27.0 mwaka 2025 hadi asilimia 23.6 mwaka 2026, wakati Wilaya za Chakechake na Magharibi B zilionyesha ongezeko kubwa la usajili wa vifo katika mwaka 2026.

**Jadweli Na. 12: Mlinganisho wa Vifo vilivyosajiliwa Aprili – Juni, 2025, 2026 na Aprili – Juni, 2026**

| Wilaya | Aprili-Juni, 2025 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 19 | 16 | **35** | 32 | 16 | **48** |
| Kaskazini B | 10 | 2 | **12** | 16 | 9 | **25** |
| Kati | 19 | 22 | **41** | 18 | 11 | **29** |
| Kusini | 18 | 9 | **27** | 9 | 8 | **17** |
| Mjini | 85 | 41 | **126** | 84 | 45 | **129** |
| Magharibi A | 28 | 17 | **45** | 27 | 24 | **51** |
| Magharibi B | 12 | 22 | **34** | 45 | 23 | **68** |
| Micheweni | 18 | 6 | **24** | 22 | 10 | **32** |
| Wete | 21 | 5 | **26** | 13 | 15 | **28** |
| Chakechake | 25 | 21 | **46** | 44 | 25 | **69** |
| Mkoani | 30 | 21 | **51** | 36 | 15 | **51** |
| **Jumla** | **285** | **182** | **467** | **346** | **201** | **547** |

## 2.2 Usajili wa Vifo Ndani ya Wakati

Kwa kipindi cha Aprili hadi Juni 2026, jumla ya vifo 481 vilisajiliwa ndani ya wakati, ambapo wanaume walikuwa 308 sawa na asilimia 64.0 na wanawake walikuwa 173 sawa na asilimia 36.0, hali inayoonesha kuwa vifo vya wanaume vilikuwa vingi zaidi kuliko vya wanawake katika kipindi hicho. Kwa mujibu wa miezi, Aprili ilisajili vifo 173, sawa na asilimia 36.0 ya vifo vyote, wakiwemo wanaume 112 (64.7%) na wanawake 61 (35.3%). Mei ilisajili vifo 179, sawa na asilimia 37.2, ambapo wanaume walikuwa 114 (63.7%) na wanawake 65 (36.3%). Aidha, Juni ilisajili vifo 129, sawa na asilimia 26.8, ukiwemo wanaume 82 (63.6%) na wanawake 47 (36.4%). Takwimu hizi zinaonesha kuwa usajili wa vifo uliongezeka kwa kiwango kidogo kutoka Aprili hadi Mei, kisha ukapungua kwa kiasi kikubwa mwezi Juni, huku wanaume wakiendelea kuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika miezi yote mitatu.

Kwa ngazi ya wilaya, Wilaya ya Mjini ilisajili vifo vingi zaidi 124, sawa na asilimia 25.8 ya vifo vyote vilivyosajiliwa, ikifuatiwa na Magharibi B vifo 63 (13.1%), Chakechake vifo 53 (11.0%), Mkoani vifo 47 (9.8%), Kaskazini A vifo 44 (9.1%), na Magharibi A vifo 42 (8.7%). Wilaya nyingine zilikuwa Kati vifo 27 (5.6%), Micheweni vifo 23 (4.8%), Kaskazini B vifo

21 (4.4%), Wete vifo 20 (4.2%), na Kusini vifo 17 (3.5%), ambayo ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya vifo vilivyosajiliwa (Jadweli Na. 13).

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha tofauti za kijiografia katika usajili wa vifo ndani ya wakati, huku Wilaya ya Mjini ikiendelea kuwa na mchango mkubwa zaidi katika jumla ya vifo vilivyosajiliwa. Aidha, wanaume waliendelea kuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika usajili wa vifo katika kipindi chote cha Aprili hadi Juni 2026, na mwezi Mei ulikuwa na idadi kubwa zaidi ya vifo vilivyosajiliwa kuliko Aprili na Juni. Pia, takwimu zinaonesha kuwa robo ya vifo vyote vilivyosajiliwa ndani ya wakati vilitokea Wilaya ya Mjini, jambo linaloashiria mkusanyiko mkubwa wa matukio ya vifo katika wilaya hiyo ikilinganishwa na wilaya nyingine.

**Jadweli Na. 13: Usajili wa Vifo Ndani ya Wakati kwa Jinsi na Wilaya, Aprili-Juni, 2026**

| Wilaya | Aprili-2026 | | | Mei-2026 | | | Juni-2026 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 10 | 6 | **16** | 11 | 3 | **14** | 119 | 4 | **14** | 140 | 13 | **44** |
| Kaskazini B | 5 | 5 | **10** | 6 | 2 | **8** | 2 | 1 | **3** | 13 | 8 | **21** |
| Kati | 3 | 3 | **6** | 7 | 4 | **11** | 7 | 3 | **10** | 17 | 10 | **27** |
| Kusini | 4 | 3 | **7** | 2 | 2 | **4** | 3 | 3 | **6** | 9 | 8 | **17** |
| Mjini | 26 | 13 | **39** | 33 | 19 | **52** | 22 | 11 | **33** | 81 | 43 | **124** |
| Magharibi A | 11 | 6 | **17** | 8 | 7 | **15** | 5 | 5 | **10** | 24 | 18 | **42** |
| Magharibi B | 20 | 12 | **32** | 14 | 7 | **21** | 7 | 3 | **10** | 41 | 22 | **63** |
| Micheweni | 4 | 2 | **6** | 8 | 5 | **13** | 3 | 1 | **4** | 15 | 8 | **23** |
| Wete | 2 | | **2** | 3 | 5 | **8** | 5 | 5 | **10** | 10 | 10 | **20** |
| Chakechake | 15 | 8 | **23** | 8 | 7 | **15** | 11 | 4 | **15** | 34 | 19 | **53** |
| Mkoan | 12 | 3 | **15** | 14 | 4 | **18** | 7 | 7 | **14** | 33 | 14 | **47** |
| **Jumla** | **112** | **61** | **173** | **114** | **65** | **179** | **82** | **47** | **129** | **308** | **173** | **481** |

### 2.2.1 Mlinganisho wa Usajili wa Vifo ndani ya wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari – Machi, 2026 na Aprili-Juni, 2026

Jadweli Na. 14 linaonesha kuwa kwa kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya vifo 564 vilisajiliwa ndani ya wakati, ambapo wanaume walikuwa 356 (63.1%) na wanawake 208 (36.9%), hali inayoonesha kuwa vifo vya wanaume vilikuwa vingi zaidi kuliko vya wanawake. Wilaya ya Mjini iliongoza kwa kusajili vifo 133 (23.6%), ikifuatiwa na Kaskazini

A 60 (10.6%), Magharibi B 56 (9.9%), Wete 53 (9.4%), na Magharibi A 52 (9.2%), huku Wilaya ya Kaskazini B ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vifo 13 (2.3%).

Katika kipindi cha Aprili–Juni 2026, jumla ya vifo 481 vilisajiliwa ndani ya wakati, sawa na upungufu wa vifo 83 (14.7%) ikilinganishwa na kipindi cha Januari–Machi 2026. Katika kipindi hicho, wanaume walikuwa 308 (64.0%) na wanawake 173 (36.0%), hali inayoonesha kuwa wanaume waliendelea kuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika usajili wa vifo. Wilaya ya Mjini iliendelea kuongoza kwa kusajili vifo 124 (25.8%), ikifuatiwa na Magharibi B 63 (13.1%), Chakechake 53 (11.0%) na Mkoani 47 (9.8%), huku Wilaya ya Kusini ikiwa na idadi ndogo zaidi ya vifo 17 (3.5%).

Takwimu zinaonesha kuwa usajili wa vifo ndani ya wakati ulipungua kwa vifo 83, sawa na asilimia 14.7, katika kipindi cha Aprili–Juni 2026 ikilinganishwa na kipindi cha Januari–Machi 2026. Aidha, wanaume waliendelea kuwa na idadi kubwa zaidi ya vifo vilivyosajiliwa katika vipindi vyote viwili. Wilaya ya Mjini iliendelea kuwa na mchango mkubwa zaidi wa vifo vilivyosajiliwa ndani ya wakati katika vipindi vyote, ingawa idadi yake ilipungua kutoka vifo 133 hadi 124. Vilevile, baadhi ya wilaya zilionyesha mabadiliko makubwa katika usajili wa vifo, ambapo Chakechake iliongezeka kutoka vifo 43 hadi 53, na Magharibi B kutoka 56 hadi 63, wakati Wete ilipungua kwa kiasi kikubwa kutoka vifo 53 hadi 20, na Kusini kutoka 46 hadi 17. Mabadiliko haya yanaashiria tofauti za mwenendo wa usajili wa vifo kati ya wilaya katika vipindi hivi viwili.

**Jadweli Na. 14: Mlinganisho wa Usajili wa Vifo ndani ya wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari – Machi, 2026 na Aprili-Juni, 2026**

| Wilaya | Januari-Machi, 2026 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 42 | 18 | **60** | 140 | 13 | **44** |
| Kaskazini B | 9 | 4 | **13** | 13 | 8 | **21** |
| Kati | 22 | 10 | **32** | 17 | 10 | **27** |
| Kusini | 22 | 24 | **46** | 9 | 8 | **17** |
| Mjini | 85 | 48 | **133** | 81 | 43 | **124** |
| Magharibi A | 35 | 17 | **52** | 24 | 18 | **42** |
| Magharibi B | 30 | 26 | **56** | 41 | 22 | **63** |
| Micheweni | 19 | 9 | **28** | 15 | 8 | **23** |
| Wete | 36 | 17 | **53** | 10 | 10 | **20** |
| Chakechake | 22 | 21 | **43** | 34 | 19 | **53** |
| Mkoani | 34 | 14 | **48** | 33 | 14 | **47** |
| **Jumla** | **356** | **208** | **564** | **308** | **173** | **481** |

### 2.2.2 Usajili wa Vifo Nje ya Wakati

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni 2026, jumla ya vifo 66 vilisajiliwa nje ya wakati, ambapo wanaume walikuwa 38 sawa na asilimia 57.6 na wanawake walikuwa 28 sawa na asilimia 42.4. Hali hii inaonesha kuwa vifo vya wanaume vilikuwa vingi zaidi kuliko vya wanawake katika usajili wa vifo nje ya wakati. Kwa mujibu wa miezi, Aprili ilisajili vifo 24, sawa na asilimia 36.4 ya vifo vyote vilivyosajiliwa nje ya wakati, wakiwemo wanaume 15 (62.5%) na wanawake 9 (37.5%). Mei ilisajili vifo 13, sawa na asilimia 19.7, ambapo wanaume walikuwa 9 (69.2%) na wanawake 4 (30.8%). Aidha, Juni ilisajili vifo 29, sawa na asilimia 43.9, wakiwemo wanaume 14 (48.3%) na wanawake 15 (51.7%), ikiwa ni mwezi pekee ambao wanawake walizidi wanaume katika usajili wa vifo nje ya wakati.

Kwa ngazi ya wilaya, Wilaya ya Chakechake ilisajili vifo vingi zaidi 16, sawa na asilimia 24.2 ya vifo vyote vilivyosajiliwa nje ya wakati, ikifuatiwa na Micheweni vifo 9 (13.6%), Magharibi A vifo 9 (13.6%) na Wete vifo 8 (12.1%). Wilaya za Kaskazini A, Kaskazini B, na Mkoani kila moja ilisajili vifo 4 (6.1%), huku Kati ikisajili vifo 2 (3.0%). Wilaya ya Kusini haikusajili kifo chochote nje ya wakati katika kipindi hiki (Jadweli Na. 15).

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa usajili wa vifo nje ya wakati ulikuwa mdogo ukilinganishwa na usajili wa vifo ndani ya wakati. Aidha, wanaume waliendelea kuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika jumla ya usajili wa vifo nje ya wakati, ingawa mwezi Juni wanawake walikuwa wengi zaidi kuliko wanaume. Vilevile, Wilaya ya Chakechake ilikuwa na mchango mkubwa zaidi katika usajili wa vifo nje ya wakati, wakati Wilaya ya Kusini haikuwa na usajili wa vifo nje ya wakati kwa robo ya pili 2026.

**Jadweli Na. 15: Usajili wa Vifo Nje ya Wakati kwa Jinsi na Wilaya, Januari – Machi, 2026**

| Wilaya | Aprili-2026 | | | Mei-2026 | | | Juni-2026 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 0 | 2 | **2** | 1 | 0 | **1** | 119 | 1 | **1** | 120 | 3 | **4** |
| Kaskazini B | 1 | 1 | **2** | 2 | 0 | **2** | 0 | 0 | **0** | 3 | 1 | **4** |
| Kati | 1 | 0 | **1** | 0 | 0 | **0** | 0 | 1 | **1** | 1 | 1 | **2** |
| Kusini | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** |
| Mjini | 1 | 1 | **2** | 1 | 0 | **1** | 1 | 1 | **2** | 3 | 2 | **5** |
| Magharibi A | 2 | 2 | **4** | 1 | 1 | **2** | 0 | 3 | **3** | 3 | 6 | **9** |
| Magharibi B | 2 | 1 | **3** | 1 | 0 | **1** | 1 | 0 | **1** | 4 | 1 | **5** |
| Micheweni | 0 | 0 | **0** | 1 | 0 | **1** | 6 | 2 | **8** | 7 | 2 | **9** |
| Wete | 2 | 1 | **3** | 0 | 1 | **1** | 1 | 3 | **4** | 3 | 5 | **8** |
| Chakechake | 6 | 1 | **7** | 2 | 2 | **4** | 2 | 3 | **5** | 10 | 6 | **16** |
| Mkoan | 0 | 0 | **0** | 0 | 0 | **0** | 3 | 1 | **4** | 3 | 1 | **4** |
| **Jumla** | **15** | **9** | **24** | **9** | **4** | **13** | **14** | **15** | **29** | **38** | **28** | **66** |

### 2.1.3 Mlinganisho wa Vifo vilivyosajiliwa Nje ya Wakati, Januari – Machi, 2026 na Aprili-juni, 2026

Jadweli Na. 16 linaonesha kuwa katika kipindi cha Januari–Machi 2026, jumla ya vifo 91 vilisajiliwa nje ya wakati, ambapo wanaume walikuwa 61 (67.0%) na wanawake 30 (33.0%), hali inayoonesha kuwa vifo vya wanaume vilikuwa vingi zaidi kuliko vya wanawake. Wilaya ya Chakechake iliongoza kwa kusajili vifo 18 (19.8%), ikifuatiwa na Magharibi B 16 (17.6%), Magharibi A 14 (15.4%), Mjini 9 (9.9%), na Wete 9 (9.9%), huku Wilaya ya Kusini ikiwa na idadi ndogo zaidi ya kifo 1 (1.1%).

Katika kipindi cha Aprili–Juni 2026, jumla ya vifo 66 vilisajiliwa nje ya wakati, sawa na upungufu wa vifo 25 (27.5%) ikilinganishwa na kipindi cha Januari–Machi 2026. Katika kipindi hicho, wanaume walikuwa 38 (57.6%) na wanawake 28 (42.4%), hali inayoonesha kuwa wanaume waliendelea kuwa wengi zaidi kuliko wanawake katika usajili wa vifo nje ya wakati, ingawa tofauti kati ya jinsi ilipungua. Wilaya ya Chakechake iliendelea kuongoza kwa kusajili vifo 16 (24.2%), ikifuatiwa na Magharibi A 9 (13.6%), Micheweni 9 (13.6%) na Wete 8 (12.1%), huku Wilaya ya Kusini ikiwa haikusajili kifo chochote (0.0%) katika kipindi hicho.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa usajili wa vifo nje ya wakati ulipungua kwa vifo 25, sawa na asilimia 27.5, kwa kipindi cha Aprili–Juni 2026 ikilinganishwa na Januari–Machi 2026. Aidha, wanaume waliendelea kuwa na idadi kubwa zaidi ya vifo vilivyosajiliwa nje ya wakati katika vipindi vyote viwili, ingawa uwiano wa wanawake uliongezeka kutoka asilimia 33.0 hadi asilimia 42.4. Wilaya ya Chakechake iliendelea kuwa na mchango mkubwa zaidi wa usajili wa vifo nje ya wakati katika vipindi vyote viwili, wakati Wilaya ya Kusini ilisajili kifo kimoja tu kwa Januari–Machi na haikusajili kifo chochote katika Aprili–Juni 2026. Takwimu hizi zinaashiria kuimarika kwa usajili wa vifo ndani ya muda uliowekwa pamoja na kupungua kwa usajili wa vifo nje ya wakati katika kipindi cha pili cha mwaka 2026.

**Jadweli Na. 16: Mlinganisho wa Vifo vilivyosajiliwa Nje ya Wakati, Januari – Machi, 2026 na Aprili-Juni, 2026**

| Wilaya | Januari-Machi, 2026 | | | Aprili-Juni, 2026 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'me | W'ke | Jumla | W'me | W'ke | Jumla |
| Kaskazini A | 5 | 2 | **7** | 120 | 3 | **4** |
| Kaskazini B | 1 | 2 | **3** | 3 | 1 | **4** |
| Kati | 3 | 3 | **6** | 1 | 1 | **2** |
| Kusini | 0 | 1 | **1** | 0 | 0 | **0** |
| Mjini | 6 | 3 | **9** | 3 | 2 | **5** |
| Magharibi A | 11 | 3 | **14** | 3 | 6 | **9** |
| Magharibi B | 8 | 8 | **16** | 4 | 1 | **5** |
| Micheweni | 6 | 0 | **6** | 7 | 2 | **9** |
| Wete | 8 | 1 | **9** | 3 | 5 | **8** |
| Chakechake | 12 | 6 | **18** | 10 | 6 | **16** |
| Mkoani | 1 | 1 | **2** | 3 | 1 | **4** |
| **Jumla** | **61** | **30** | **91** | **38** | **28** | **66** |

## 2.3 Usajili wa Ndoa

Jadweli Na. 17 linaonesha kuwa katika kipindi cha Aprili–Juni 2026, jumla ya ndoa 336 zilisajiliwa. Kwa mujibu wa miezi, Aprili ilisajili ndoa 153 (45.5%), Mei ilisajili ndoa 54 (16.1%), na Juni ilisajili ndoa 129 (38.4%). Takwimu hizi zinaonesha kuwa mwezi Aprili ulikuwa na idadi kubwa zaidi ya usajili wa ndoa, ukifuatiwa na mwezi Juni, huku Mei ukiwa

na idadi ndogo zaidi ya usajili. Kwa ujumla, mwelekeo unaonesha kupungua kwa kiasi kikubwa kwa usajili wa ndoa kutoka Aprili hadi Mei, kisha kuongezeka tena mwezi Juni.

Kwa ngazi ya wilaya, Magharibi B iliongoza kwa kusajili ndoa 136 (40.5%), ikifuatiwa na Magharibi A 70 (20.8%), Mjini 51 (15.2%) na Kati 17 (5.1%), huku Micheweni pamoja na Mkoani, kila moja ikisajili ndoa 4 (1.2%), ambazo zilikuwa na idadi ndogo zaidi ya usajili wa ndoa katika kipindi hicho.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa usajili wa ndoa katika kipindi cha Aprili–Juni 2026 ulijikita zaidi katika Wilaya za Magharibi B na Magharibi A, ambazo kwa pamoja zilichangia ndoa 206, sawa na asilimia 61.3 ya usajili wote. Aidha, mwelekeo wa usajili wa kila mwezi unaonesha kushuka kwa kiwango kikubwa mwezi Mei kabla ya kuongezeka tena mwezi Juni, hali inayoashiria kuwa usajili wa ndoa haukuwa na mwelekeo thabiti katika kipindi hicho.

**Jadweli Na. 17: Usajili wa Ndoa kwa Wilaya, Aprili-Juni, 2026**

| Wilaya | Apr-2026 | Mei-2026 | Juni-2026 | April-Juni, 2026 |
|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 5 | 3 | 2 | 10 |
| Kaskazini B | 5 | 1 | 8 | 14 |
| Kati | 7 | 1 | 9 | 17 |
| Kusini | 1 | | 7 | 8 |
| Mjini | 26 | 9 | 16 | 51 |
| Magharibi A | 53 | 5 | 12 | 70 |
| Magharibi B | 39 | 31 | 66 | 136 |
| Micheweni | 3 | 0 | 1 | 4 |
| Wete | 7 | 2 | 3 | 12 |
| Chakechake | 6 | 1 | 3 | 10 |
| Mkoani | 1 | 1 | 2 | 4 |
| **Jumla** | **153** | **54** | **129** | **336** |

### 2.3.1 Mlinganisho wa Usajili wa Ndoa, Januari–Machi, 2026 na Aprili-Juni, 2026

Jadweli Na. 18 linaonesha kuwa katika kipindi cha Aprili–Juni 2026 zilisajiliwa jumla ya ndoa 336, ikilinganishwa na ndoa 288 zilizosajiliwa katika kipindi cha Januari–Machi 2026. Hii ni ongezeko la ndoa 48, sawa na asilimia 16.7, jambo linaloonesha kuimarika kwa usajili wa ndoa katika robo ya pili ya mwaka.

Kwa ngazi ya wilaya, Magharibi B ilirekodi ongezeko kubwa zaidi la usajili wa ndoa kutoka 40 hadi 136, sawa na ongezeko la ndoa 96 (240.0%). Aidha, Mjini iliongezeka kutoka ndoa 44 hadi 51 (15.9%), Kaskazini A kutoka 0 hadi 10 na Kaskazini B kutoka 0 hadi 14. Baadhi ya wilaya zilionesha kupungua kwa usajili wa ndoa ambapo Magharibi A ilishuka kutoka ndoa 144 hadi 70, ikiwa ni punguzo la ndoa 74 (51.4%), huku Kusini ikishuka kutoka ndoa 36 hadi 8, sawa na punguzo la ndoa 28 (77.8%).

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa licha ya ongezeko la jumla la usajili wa ndoa katika kipindi cha Aprili–Juni 2026, mwenendo huo haukuwa sawa katika wilaya zote. Ongezeko kubwa lilitokana zaidi na kuimarika kwa usajili katika Wilaya ya Magharibi B, pamoja na kuanza kwa usajili katika wilaya ambazo hazikuwa zimesajili ndoa yoyote katika kipindi cha Januari–Machi (Kaskazini A, Kaskazini B, Micheweni na Mkoani). Hata hivyo, kupungua kwa usajili katika Magharibi A na Kusini kunaonesha kuwa kulikuwa na tofauti za mwenendo wa usajili wa ndoa kati ya wilaya katika robo hizo mbili za mwaka.

**Jadweli Na. 18: Mlinganisho wa Usajili wa Ndoa, Januari – Machi, 2026 na Aprili-Juni, 2026**

| Wilaya | Januari- Machi, 2026 | April-Juni, 2026 |
|---|---|---|
| Kaskazini A | 0 | 10 |
| Kaskazini B | 0 | 14 |
| Kati | 12 | 17 |
| Kusini | 36 | 8 |
| Mjini | 44 | 51 |
| Magharibi A | 144 | 70 |
| Magharibi B | 40 | 136 |
| Micheweni | 0 | 4 |
| Wete | 4 | 12 |
| Chakechake | 8 | 10 |
| Mkoani | 0 | 4 |
| **Jumla** | **288** | **336** |

## 2.4 Usajili wa Talaka

Jadweli Na. 19 linaonesha kuwa katika kipindi cha Aprili–Juni 2026, jumla ya talaka 100 zilisajiliwa. Kati ya hizo, mwezi Mei uliongoza kwa kusajili talaka 46 (46.0%), ukifuatiwa na Juni wenye talaka 32 (32.0%), na Aprili wenye talaka 22 (22.0%). Takwimu hizi

zinaonesha kuwa usajili wa talaka uliongezeka kutoka Aprili hadi kufikia kiwango cha juu mwezi Mei, kisha ukapungua mwezi Juni.

Kwa ngazi ya wilaya, Magharibi B iliongoza kwa kusajili talaka 54 (54.0%) ya talaka zote zilizosajiliwa katika kipindi hicho, ikifuatiwa na Mjini na Magharibi A, ambazo kila moja ilisajili talaka 16 (16.0%). Kusini na Chakechake kila moja zilisajili talaka 4 (4.0%), huku Kaskazini A, Kaskazini B, na Kati kila moja ikisajili talaka 2 (2.0%).

Aidha, Wilaya za Micheweni, Wete na Mkoani hazikusajili talaka yoyote (0) katika kipindi chote cha Aprili–Juni 2026. Vilevile, baadhi ya wilaya zilikuwa na miezi ambayo haikusajili talaka yoyote. Kaskazini A na Kaskazini B hazikusajili talaka mwezi Mei na Juni, Kati haikusajili talaka mwezi Aprili na Mei, Kusini haikusajili talaka mwezi Juni, na Mjini haikusajili talaka mwezi Juni.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa usajili wa talaka katika kipindi cha Aprili–Juni 2026 ulijikita zaidi katika Wilaya ya Magharibi B, ambayo peke yake ilichangia zaidi ya nusu (54.0%) ya talaka zote zilizosajiliwa. Mwelekeo wa usajili unaonesha kuongezeka kwa talaka kutoka Aprili hadi Mei kabla ya kupungua mwezi Juni, huku kutokuwepo kwa usajili wa talaka katika baadhi ya wilaya kukiashiria tofauti za mwenendo wa talaka na matumizi ya huduma za usajili kati ya wilaya za Zanzibar.

**Jadweli Na. 19: Usajili wa Talaka kwa Mwezi Aprili Juni, 2026**

| Wilaya | Apr-26 | Mei-2026 | Juni-2026 | April-Juni, 2026 |
|---|---|---|---|---|
| Kaskazini A | 2 | 0 | 0 | 2 |
| Kaskazini B | 2 | 0 | 0 | 2 |
| Kati | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Kusini | 2 | 2 | 0 | 4 |
| Mjini | 2 | 14 | 0 | 16 |
| Magharibi A | 8 | 2 | 6 | 16 |
| Magharibi B | 6 | 26 | 22 | 54 |
| Micheweni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wete | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 0 | 2 | 2 | 4 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **22** | **46** | **32** | **100** |

### 2.4.1 Mlinganisho wa Usajili wa Talaka kwa Januari–Machi, 2026 na April-Juni 2026

Jadweli Na. 20 linaonesha kuwa katika kipindi cha Aprili–Juni 2026 zilisajiliwa jumla ya talaka 100, ikilinganishwa na talaka 144 zilizosajiliwa katika kipindi cha Januari–Machi 2026. Hii ni punguzo la talaka 44, sawa na asilimia 30.6, jambo linaloonesha kupungua kwa usajili wa talaka katika robo ya pili ya mwaka.

Kwa ngazi ya wilaya, Magharibi B ndiyo wilaya pekee iliyorekodi ongezeko kubwa la usajili wa talaka, kutoka talaka 20 hadi 54, sawa na ongezeko la talaka 34 (170.0%). Aidha, Kaskazini A na Kaskazini B ziliongezeka kutoka talaka 0 hadi 2 kila moja, wakati Chakechake ilibaki na kiwango kilekile cha talaka 4 katika vipindi vyote viwili. Kwa upande mwingine, wilaya nyingi zilionesha kupungua kwa usajili wa talaka na nyengine kutokusajili kabisa kwa kipindi cha Aprili–Juni 2026.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa usajili wa talaka ulipungua katika robo ya pili ya mwaka 2026, licha ya ongezeko kubwa lililorekodiwa katika Wilaya ya Magharibi B. Kupungua kwa usajili katika wilaya nyingi, hususan Magharibi A, Kusini, na Mjini, ndiko kulikochangia zaidi kushuka kwa idadi ya talaka zilizosajiliwa kutoka 144 hadi 100 kati ya vipindi hivyo viwili. Hali hii inaonesha kuwa mwenendo wa usajili wa talaka ulitofautiana kati ya wilaya, huku baadhi zikiongeza usajili na nyingine zikionesha upungufu mkubwa.

**Jadweli Na. 20: Mlinganisho wa Usajili wa Talaka kwa Januari–Machi, 2026 na April-Juni 2026**

| Wilaya | Januari- Machi, 2026 | April-Juni, 2026 |
|---|---|---|
| Kaskazini A | 0 | 2 |
| Kaskazini B | 0 | 2 |
| Kati | 6 | 2 |
| Kusini | 18 | 4 |
| Mjini | 22 | 16 |
| Magharibi A | 72 | 16 |
| Magharibi B | 20 | 54 |
| Micheweni | 0 | 0 |
| Wete | 2 | 0 |
| Chakechake | 4 | 4 |
| Mkoani | 0 | 0 |
| **Jumla** | **144** | **100** |

### 2.4.2 Uhusiano na Mwenendo wa Ndoa na Talaka katika kipindi cha Aprili–Juni 2026

Uhusiano kati ya usajili wa ndoa na talaka katika kipindi cha Aprili–Juni 2026 unaonesha kuwa katika kipindi hicho zilisajiliwa jumla ya ndoa 336 na talaka 100 Zanzibar. Kwa ujumla, wilaya zilizosajili idadi kubwa ya ndoa pia zilikuwa miongoni mwa wilaya zilizosajili idadi kubwa ya talaka, ingawa uwiano huo haukuwa sawa katika wilaya zote.

Kwa ngazi ya wilaya, Magharibi B iliongoza kwa kusajili ndoa 136 na pia ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya talaka 54, ikifuatiwa na Magharibi A yenye ndoa 70 na talaka 16, pamoja na Mjini iliyosajili ndoa 51 na talaka 16. Kati ilisajili ndoa 17 na talaka 2, huku Kaskazini B ikiwa na ndoa 14 na talaka 2, na Kaskazini A ikiwa na ndoa 10 na talaka 2. Kusini ilisajili ndoa 8 na talaka 4, idadi ambayo inaonesha uwiano mkubwa wa talaka ikilinganishwa na ndoa zilizosajiliwa katika wilaya hiyo.

Kwa upande mwingine, wilaya zilizokuwa na kiwango kidogo cha usajili wa ndoa pia zilionesha idadi ndogo au kutokuwepo kabisa kwa usajili wa talaka. Micheweni, Wete, na Mkoani zilisajili ndoa 4, 12, na 4 mtawalia, lakini hazikusajili talaka yoyote katika kipindi hicho. Aidha, Chakechake ilisajili ndoa 10 na talaka 4, hali inayoonesha kuwa licha ya kuwa na idadi ndogo ya ndoa, usajili wa talaka ulikuwepo.

Kwa ujumla, takwimu zinaonesha kuwa kuna uhusiano wa karibu kati ya usajili wa ndoa na talaka, ambapo wilaya zenye shughuli nyingi za usajili wa ndoa, hususan Magharibi B, Magharibi A, na Mjini, pia zilirekodi idadi kubwa ya talaka. Hata hivyo, tofauti za uwiano kati ya ndoa na talaka katika baadhi ya wilaya, kama Kusini na Chakechake, pamoja na kutokuwepo kwa talaka katika Micheweni, Wete, na Mkoani licha ya kuwepo kwa usajili wa ndoa, zinaonesha kuwa kiwango cha usajili wa ndoa pekee hakitoshi kuelezea mwenendo wa talaka. Hivyo, kuna uwezekano wa kuwepo kwa sababu nyingine za kijamii, kiuchumi au kiutawala zinazoathiri mwenendo wa talaka katika wilaya mbalimbali (Jadweli Na. 21).

**Jadweli Na. 21: Uhusiano na Mwenendo wa Ndoa na Talaka kwa Aprili–Juni, 2026**

| Wilaya | Aprili-Juni 2026 | |
|---|---|---|
| | Ndoa | Talaka |
| Kaskazini A | 10 | 2 |
| Kaskazini B | 14 | 2 |
| Kati | 17 | 2 |
| Kusini | 8 | 4 |
| Mjini | 51 | 16 |
| Magharibi A | 70 | 16 |
| Magharibi B | 136 | 54 |
| Micheweni | 4 | 0 |
| Wete | 12 | 0 |
| Chakechake | 10 | 4 |
| Mkoani | 4 | 0 |
| **Jumla** | **336** | **100** |

## 3.0 Hitimisho

Kwa ujumla, takwimu za matukio ya kijamii zina mchango mkubwa katika kuimarisha upangaji, utekelezaji na tathmini ya mipango ya maendeleo pamoja na kuboresha utoaji wa huduma za kijamii nchini. Usajili sahihi na wa wakati wa matukio ya kijamii, ikiwemo vizazi, vifo, ndoa na talaka, huiwezesha Serikali na wadau wa maendeleo kupata takwimu za kuaminika zinazotumika katika kufanya maamuzi sahihi ya kisera, ugawaji wa rasilimali na ufuatiliaji wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Taarifa hii imewasilisha takwimu za matukio ya kijamii yaliyosajiliwa rasmi kupitia Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) katika kipindi husika. Hata hivyo, bado yapo matukio mengi yanayotokea katika jamii ambayo hayasajiliwi rasmi, hususan vifo, ndoa na talaka. Hali hii husababisha kutokuwepo kwa takwimu kamili na sahihi, jambo linaloweza kuathiri ubora wa mipango na maamuzi yanayotegemea taarifa hizo.

Kwa kuzingatia umuhimu wa takwimu hizi, jamii inahimizwa kuendelea kujenga utamaduni wa kusajili matukio yote ya kijamii kwa wakati na kwa mujibu wa sheria. Hatua hiyo itachangia kuongeza ukamilifu na ubora wa takwimu rasmi, hivyo kuiwezesha Serikali na wadau wa maendeleo kupanga, kutekeleza na kutathmini mipango mbalimbali

kwa ufanisi zaidi, kwa lengo la kuimarisha ustawi wa wananchi na kufikia malengo ya maendeleo endelevu.

### Maelezo Muhimu

- Kizazi hai ni tukio la mtoto kuzaliwa akiwa hai, yaani, mtoto ambaye amezaliwa ana pumzi, anafanya harakati, na ana ishara za maisha. Kizazi hai mara nyingi hufuatana na mchakato wa kawaida wa kujifungua, ambapo mtoto huzaliwa kuja ulimwenguni.

- Kifo ni tukio la mwisho la kuishi. Ni tukio ambalo mwili huacha kabisa kufanya kazi kwa binadamu, kifo hutokea wakati moyo unasimama na kusitisha mtiririko wa damu mwilini, na ubongo kusimama kufanya kazi.

- Usajili ndani ya wakati ni usajili wa matukio muhimu kama vile vizazi, vifo, ndoa au talaka ndani ya muda uliowekwa kisheria baada ya tukio kutokea.

- Usajili nje ya wakati ni usajili wa matukio kama vile vizazi, vifo, ndoa au talaka kusajiliwa baada ya muda uliowekwa kisheria kupita.

- Ndoa ni muungano wa kisheria na kijamii kati ya watu wawili unaotambuliwa na sheria, mila au dini, kwa lengo la kuishi pamoja kama mume na mke na kuunda familia.

- Talaka ni kitendo cha kisheria cha kuvunja au kusitisha ndoa halali, ambapo wanandoa hawatambuliki tena kama mume na mke mbele ya sheria, dini au jamii.

- Sheria Namba 3 ya 2018, inaeleza kuwa Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) ina majukumu ya kusajili Matukio ya kijamii na kutoa vyeti maalum, matukio hayo ni Vizazi, Vifo, Ndoa, Talaka na Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na Wasiokua Wazanzibari Wakaazi.

- Sheria Namba 9 ya mwaka 2007 inaeleza kuwa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar ina mamlaka ya kuratibu na kusimamia uendeshaji wa kazi za takwimu katika taasisi zote za Serikali na binafsi zinazofanya shughuli zake hapa Zanzibar.

*Kwa Ufafanuzi Zaidi Tafadhali Wasiliana na:*

**OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI,**
S.L.P 2321, 7 Barabara ya Fumba, 71125 Mjini Magharibi,
Zanzibar – Tanzania.
Simu  +255 24 2231869
Faksi: +255 24 2231742
Barua pepe: cgs@ocgs.go.tz
Website: www.ocgs.go.tz

**WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMI**
Simu: +255 772 400 597
S.L.P: 264
Barua pepe: info@zcsra.go.tz
Flamingo, Migombani Zanzibar Tanzania.